

Nini cha kufanya ikiwa mtu kazini ana COVID-19

Ikiwa mtu kazini ana COVID-19, au amehatarishwa kuipata, utahitaji kufuata hatua hapa chini mara moja. Usingoje hadi ithibitishwe kuwa ana COVID-19.

Habari hii ni kukusaidia katika mahali pa kazi. Hata hivyo, unapaswa kila wakati kufuata ushauri wa [idara ya afya ya umma ya jimbo lako au wilaya \(state or territory public health department\)](#).

Ikiwa mtu ana dalili mbaya kama vile ugumu wa kupumua, pigia simu 000.

1. Tenga mtu huyo

Tenga mtu huyo kutoka kwa wengine. Unapaswa pia kuwapatia, na kila mtu anayemsaidia, na vifaa vya kinga vya kibinafsi kama mask ya upasuaji na matibabu ya sanitaiza ya mkono

2. Tafuta ushauri na tathmini hatari

Tafuta ushauri wa kiafya wa serikali kutoka kwa [simu ya msaada ya jimbo lako au wilaya \(state or territory helpline\)](#), au Nambari ya Msaada ya Kitaifa ya virusi vya Corona (1800 020 080).

Hakikisha una habari ya mawasiliano ya mtu huyo. Andika kumbukumbu juu ya maeneo ambayo amekuwepo katika eneo la kazi, nani ambaye alikuwa akiwasiliana sana, na kwa muda gani, ili kujijulisha juu ya hatari kwa wengine na maeneo ya kusafisha na dawa ya kuua vijidudu.

Unaweza pia kuhitaji kuarifu [mrekebishaji wa hali ya afya ya jimbo lako au wilaya \(state or territory work health and safety regulator\)](#).

3. Usafiri

Hakikisha mtu huyo ana usafiri kwenda nyumbani kwake, eneo la kujitenga, au kituo cha matibabu ikiwa inahitajika. Wakati wowote inapowezekana, anapaswa kutumia usafiri wa njia ya kibinafsi ili kupunguza hatari kwa wengine.

4. Safisha na kutumia dawa ya kuua vijidudu

Funga maeneo ambayo mtu huyo ametumia mpaka yamesafishwa na kutumiwa dawa. Fungua milango ya nje na madirisha ikiwa inawezekana ili kuongeza mazunguko ya hewa.

Safisha kabisa na kuosha dawa maeneo na vifaa ambavyo mtu alivyotumia, kama ofisi, bafu, jikoni na maeneo ya kawaida.

Wanadhifishaji wanapaswa kuvaa vifaa vya kinga vya kibinafsi, kwa mfano glavu, miwani ya usalama na aproni inayoweza kutupwa.

5. Tambua na waambie wasiliano wa karibu

Kitengo cha afya cha umma ya jimbo au wilaya kitatambua watu waliokaribiana sana na kesi iliyothibitishwa ya COVID-19 na kuwaambia wanahitaji kufanya nini.

Gundua ni nani mtu huyo amekuwa akiwasiliana nao sana katika mahali pa kazi na kwa muda gani, na wapi wale waliowasiliana karibu ya mtu aliyeathiriwa wamekuwepo katika mahali pa kazi.

Hii itajjulisha juu ya hatari zinazoweza kwa wengine, na maeneo ya ziada ambayo yanaweza kuhitaji kusafisha na kutumia dawa ya kuua vijidudu.

6. Kagua udhibiti wa usimamizi wa hatari

Kagua udhibiti wako wa kusimamia hatari za COVID-19 kwa kushauriana na wafanyakazi wako na utathimini ikiwa mabadiliko yanahitajika.

Hatua za kuchukua wakati mtu ambaye unamjali naye alikuwa mahali pako pa kazi

Mtu ambaye amekuwepo kazini kwako hivi karibuni, kama mfanyakazi au mteja, anaweza kukuarifu kuwa aliweza kuwa na COVID-19. Fikiria alikuwepo lini hivi karibuni mahali pako pa kazi na ikiwa aliwasiliana sana na wengine.

Hata kama hawako kwa kisasa mahali pa kazi, bado unaweza kuhitaji kufuata hatua zilizo hapo juu. Tafuta ushauri kutoka kwa [simu ya msaada ya jimbo lako au wilaya \(state or territory helpline\)](#).

Je! Ninahitaji kufunga mahali pangu pa kazi?

Hakuna hitaji ya kiotomatiki ya kufunga eneo la kazi kufuata kesi inayoshukiwa au iliyothibitishwa na COVID-19. Inaweza kutohitajika ikiwa mtu huyo ametembelea tu sehemu za kazi yako au ikiwa maafisa wa afya wanakushauri hatari ya wengine kuhatarishwa ni kidogo.

Ikiwa eneo lako la kazi linahitaji kufunga inategemea mambo kama ukubwa, aina ya kazi, idadi ya watu na maeneo yanayoshukiwa ya uchafuzi.

Je! Ni lini wafanyakazi wanaweza kurudi kazini kufuatia kupona au karantini?

Wafanyakazi ambao wametengwa baada ya kupimwa kuwa na COVID-19 wanaweza kurudi kazini tu wakati wameshapona kabisa na kuruhusiwa na maafisa wa afya.

Wafanyakazi ambao hawakuwa na dalili zozote wakati wa kutengwa katika karantini wanaweza kurudi kazini wanapomaliza kipindi cha siku 14. Hawahitaji kibali cha matibabu ili kurudi kazini.

Habari zaidi

Kwa habari zaidi, nenda kwa [tovuti ya Kazi Salama Australia \(Safe Work Australia website\)](https://www.swa.gov.au/coronavirus)